



**TANZANIA  
BASKETBALL  
FEDERATION**

Affiliated to FIBA | FIBA AFRICA | FIBA ZONE V

National Indoor Stadium | P.O Box 42089 Dar Es Salaam | TEL: +255 713 705463 - 255 655 759097 | info@tbf.or.tz | www.tbf.or.tz

## **TAARIFA KUHUSU SHINDANO LA CRDB TAIFA CUP 2024**

**Kwa Wenyeviti,  
Mikoa yote (Tanzania Bara na Visiwani)**

Shirikisho la Mpira wa Kikapu nchini (TBF) kama wasimamizi wa mpira wa kikapu wenye jukumu la kukuza na kuendeleza mchezo nchini kwa vijana wa rika zote. Kupitia kalenda yake ya mwaka, Shirikisho lilipanga kuendesha shindano lake la kitaifa kwa mikoa liljulikanalo kama **CRDB BANK TAIFA CUP** kupitia ushirikiano na udhamini toka **Benki ya CRDB** pamoja na washirika wake. Shindano hili lilipangwa kufanyika mwishoni mwa mwezi **Februari, 2024**.

Aidha, Baada ya majadiliano kati ya Uongozi wa Shirikisho, Benki ya CRDB kupitia taasisi yake ya **CRDB BANK FOUNDATION** na wadau wengine ambao wameonyesha utayari wa kushiriki katika Taifa Cup kwa pamoja tumekubaliana kusogeza shindano la **CRDB BANK TAIFA CUP** mpaka tarehe 19 - 29 JUNE 2024 ili kupisha maandalizi ya timu ya taifa inayojiandaa kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayotarajiwa kuanza tarehe 01 – 10 Februari 2024 nchini Rwanda.

Kutokana na sababu hizo Shirikisho la Mpira wa Kikapu (TBF) linapenda kutoa **TAARIFA MUHIMU** kwa Viongozi wa Mikoa na Wadau mbalimbali kuhusu mabadiliko ya tarehe na muda wa kufanya Shindano la CRDB BANK TAIFA CUP.

Hivyo, Shirikisho linaomba mikoa shiriki kufanya taratibu zote za maandalizi kwa kushirikisha wadau wao ili kuiwezesha mikoa kushiriki bila changamoto zozote. Tunaomba radhi kwa usumbufu na changamoto zozote zitakazojitokeza kutokana na mabadiliko haya ya tarehe husika.

**IMETOLEWA  
19 JANUARI 2024**